## HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA

Mhe. Mwenyekiti,

**BARAZA LA MADIWANI**

## TAARIFA YA MKURUGENZI KATIKA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI KWA KIPINDI CHA ROBO YA PILI (OCTOBA – DISEMBA) MWAKA WA FEDHA 2024/2025 TAREHE 30/01/2025

### UTANGULIZI

**Mhe. Mwenyekiti**, Kwa mujibu wa Kanuni za kudumu za Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela za Mwaka 2014, Mkurugenzi anawajibika kulitaarifu Baraza la Madiwani kwa kutoa Taarifa ya Matukio mbalimbali ambayo yamefanyika au yanatarajia kutokea katika kipindi cha kila Robo ya Mwaka. Hivyo, Taarifa hii imegawanyika katika Maeneo yafuatayo: -

1. TAARIFA YA MAKUSANYO KWA ROBO YA PILI
2. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ROBO YA PILI

   **2.1 MAPATO YA NDANI**

   2.1 Utekelezaji wa Miradi kwa fedha za Mapato ya Ndani Bajeti ya 2024/2025 kwa robo ya pili

   **2.2 SERIKALI KUU**

   2.2.1 Mapokezi ya fedha kutoka Serikali Kuu

   2.2.2 Utekelezaji wa Miradi kwa fedha za Serikali Kuu robo ya pili

3. TAARIFA ZA MATUKIO MBALIMBALI KWA KIPINDI CHA ROBO YA PILI
4. HITIMISHO



CamScanner

**i.**

## i. 1. TAARIFA YA MAKUSANYO KWA ROBO YA PILI

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Halmashauri yetu imekusudia kukusanya kiasi cha 14,953,399,100.00 katika bajeti ya mapato ya ndani, ambapo hadi kufikia tarehe 31 Disemba mwaka wa fedha 2024/2025 Halmashauri imefanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 7,013,513,255.00 sawa na asilimia 47 ya lengo la mwaka na sawa na asilimia 93.8 ya lengo la Nusu mwaka.

## 2. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ROBO YA PILI

### 2.1 Utekelezaji wa miradi kwa fedha za mapato ya ndani bajeti ya 2024/2025

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, kwa robo ya pili, jumla ya shilingi 270,964,000.00 fedha za mapato ya ndani zilielekezwa kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwa ni utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2024/2025 kwa mchanganuo ufuatao;

i. Shilingi 70,000,000.00 kwa ajili ya ununuzi wa eneo kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Nyasaka
ii. Shilingi 25,000,000.00 kwa ajili ya ukamilishaji wa vyumba 2 vya madarasa Shule ya Msingi Magaka.
iii. Shilingi 25,000,000.00 kwa ajili ya ukamilishaji wa madarasa 2 Shule ya Msingi Chasubi
iv. Shilingi 25,000,000.00 kwa ajili ya ukamilishaji wa madarasa 2 Shule ya Msingi Mhonze
v. Shilingi 23,954,000/= kwa ajili ya ununuzi wa viti na meza 350 kwa shule za Sekondari
vi. Shilingi 23,010,000/= kwa ajili ya ununuzi wa madawati 325 katika shule za msingi awamu ya kwanza
vii. Shilingi 18,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa vyoo shule ya Sekondari Bujingwa
viii. Shilingi 18,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa vyoo shule ya Sekondari Ibinza



CamScanner

ix. Shilingi 15,000,000.00 ambayo ni malipo ya fundi kwa ajili ya utengenezaji wa vyumba(partition) katika jengo la Utawala

x. Shilingi 14,000,000.00 kwa ajili ya ukamilishaji wa vyoo shule ya Msingi Ibungilo

xi. Shilingi 14,000,000.00, kwa ajili ya ukamilishaji wa vyoo shule ya Msingi Isesa

Pamoja na miradi hii, Halmashauri imeendelea kutekeleza miradi mingine ya Maendeleo kwa fedha za mapato ya ndani yenye thamani ya shilingi **2,435,463,106.82** ambayo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji kama inavyoonekana kwenye **KIAMBATANISHO NAMBA 1.**

ka Serikali Kuu kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo katika kata zetu.

### 2.2 Utekelezaji wa Miradi kwa fedha za Serikali Kuu robo ya pili

**Mheshimiwa Mwenyekiti;** katika kipindi hiki fedha zilizopokelewa ni shilingi **966,157,000.00** na zimeelekezwa kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo katika kata zetu kwa mchanganuo ifuatao;

i. Shilingi 300,000,000.00 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba katika Hospitali ya Wilaya

ii. Shilingi 239,000,000.00 kwa ajili ya ukamilishaji wa Hospitali ya Wilaya

iii. Shilingi130,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa bweni shule ya Sekondari Bwiru Wavulana

iv. Shilingi 113,396,000.00 kwa ajili ya ukamilishaji wa Bwalo Shule ya Sekondari Sangabuye

v. Shilingi 100,000,000.00 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba Zahanati

vi. Shilingi 83,761,000.00 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi kupitia fedha za Mfuko wa Jimbo.

Pamoja na miradi hii, Halmashauri imeendelea kutekeleza miradi mingine ya Maendeleo kwa fedha za mapato kutoka Serikali Kuu yenye thamani ya shilingi **2,569,139,963.06** ambayo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji kama inavyoonekana kwenye **KIAMBATANISHO NAMBA 2.**



CS CamScanner

## 3. TAARIFA ZA MATUKIO MBALIMBALI KWA KIPINDI CHA ROBO YA PILI.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mnamo tarehe 14/10/2024 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan alifika katika Jiji la Mwanza, Wilaya ya Ilemela kwa ajili ya sherehe za kilele cha Maadhimisho ya Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa kwa mwaka 2024. Pamoja na mambo mengine, Mheshimiwa Rais alifanya uzinduzi wa kitabu cha Historia ya Mwenge wa Uhuru.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mnamo tarehe 11/10/2024 hadi 20/10/2024, Wananchi katika Halmashauri yetu waliungana na watanzania wengine katika zoezi la uandikishaji wa orodha ya wapigakura. Zoezi hili lilifanyika katika mitaa yote 171 kwenye vituo 493 vya kujiandikisha ambapo jumla ya wananchi 296,715 wakiwemo wanaume 148,936 na wanawake 147,779 sawa na 98.1% ya Lengola watu 302,770 waliandikishwa.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mnamo tarehe 13/10/2024, Mwenge wa Uhuru ulikimbizwa katika Wilaya yetu ambapo jumla ya miradi 10 yenye thamani ya shilingi 2,104,501,879.00 ilitembelewa. Kiongozi wa Mbio za Mwenge Kitaifa Ndugu Godfrey Eliakim Mnzava, ambaye pia ni Afisa Tarafa katika Tarafa ya Ilemela, alifanikiwa kujiandikisha katika orodha ya wapigakura Mtaa wa Buhilya Kata ya Buswelu. Vilevile, katika Mbio za Mwenge wa Uhuru Wilaya yetu imeshika nafasi ya tisa kitaifa, na nafasi ya tatu kikanda, na nafasi ya kwanza katika Mkoa wa Mwanza.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mnamo Tarehe 16/10/2024 Halmashauri yetu ilisaini mkataba wa ujenzi wa soko la kisasa Kirumba pamoja na ujenzi wa barabara zinazozunguka soko zenye urefu wa kilomita 2.9, unaofadhiliwa na Mradi wa uboreshaji miundombinu na Miji ya Tanzania (TACTIC). Mradi huu utatekelezwa chini ya mkandarasi M/s China Raillway 15 Bureau group Corporation, utagharimu jumla ya shilingi bilioni 14.71(bila VAT). Mradi huu umeanza kutekelezwa tarehe 1 Novemba 2024 na utamalizika tarehe 31Oktoba 2025. Aidha, hafla ya utiaji saini ilishuhudiwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa (MB).



CS CamScanner

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mnamo Tarehe 23/10/2024 hadi tarehe 24/10/2024 Jumla ya wanafunzi 14,647 wa darasa la nne walifanya mtihani wa upimaji wa Kitaifa wa darasa la nne katika shule za Msingi zilizopo katika Halmashauri yetu, ambapo katika matokeo yao, Halmashauri yetu imeshika nafasi ya kwanza ya ufaulu kimkoa na kupata wastani wa 95.1%.

Vilevile, katika kipindi hiki matokeo ya darasa la saba yalitangazwa, ambapo Halmashauri yetu imeshika nafasi ya kwanza ya ufaulu kimkoa na kupata wastani wa 93.75%

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Mnamo tarehe 28/10/2024 hadi tarehe 11/11/2024 wanafunzi wa kidato cha pili katika shule za sekondari za Halmashauri yetu walifanya mtihani wa upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha pili, ambapo katika matokeo yao, Halmashauri yetu imepata GPA ya 3.2394 sawa na ongezeko la 0.0565% , na ufaulu wa 92.2%.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Mnamo tarehe 27/11/2024 Wananchi katika Halmashauri yetu walishiriki katika zoezi la kupiga kura kwa ajili ya kuwachagua viongozi wa Serikali za Mitaa ambao ulifanyika katika kata 19, Mitaa 171 Vituo 493 vya kupigia kura. Aidha, jumla ya vyama vya Siasa 15 vilishiriki, vikiwa na jumla ya wagombea 373 wa nafasi ya Uenyekiti, na wagombea 1,425 wa nafasi ya wajumbe Kamati ya mtaa kundi mchanganyiko na kundi la wanawake.

Uchaguzi wa Serikali za Mitaa katika Halmashauri yetu ulifanyika kwa amani na utulivu, ambapo katika mitaa 171, wenyeviti 158 walioshinda sawa na 92.3% na wajumbe 853 sawa na 99.7% walitoka Chama Cha Mapinduzi, wenyeviti 12 sawa na 7.01% na wajumbe 2 sawa na 0.23% walitoka Chama cha Demokrasia na Maendeleo na mwenyekiti 1 sawa 0.58%alitoka Chama cha ACT Wazalendo.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Mnamo tarehe 09/12/2024 Halmashauri yetu ilishiriki katika maadhimisho ya miaka 63 ya Uhuru wa Tanzania Bara. Maadhimisho haya yaliambatana na shughuli za usafi wa mazingira na upandaji wa miti katika soko la Kabwalo Kata ya Buswelu na hatimaye kongamano la miaka 63 ya Uhuru lililofanyika katika viwanja vya Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela.



CamScanner

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Mnamo tarehe 09/12/2024 Halmashauri yetu ilishiriki katika maadhimisho ya miaka 63 ya Uhuru wa Tanzania Bara. Maadhimisho haya yaliambatana na shughuli za usafi wa mazingira na upandaji wa miti katika soko la Kabwalo Kata ya Buswelu na hatimaye kongamano la miaka 63 ya Uhuru lililofanyika katika viwanja vya Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Mnamo tarehe 16/12/2024 Baraza la Madiwani kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji walitembelea Halmashauri yetu na kujifunza mambo mbalimbali ikiwemo ukusanyaji wa mapato katika mazao ya samaki.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Mnamo tarehe 23/12/2024 Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi walitembelea Halmashauri yetu na kujifunza mambo mbalimbali ikiwemo uendeshaji wa vibanda vya biashara na mapato yanayotokana na mazaoya samaki.

## 4. HITIMISHO

Tunapenda kutoa shukrani za dhati kwa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutupa fedha kwa ajili ya kutekeleza Miradi mbalimbali ya maendeleo katika Halmashauri yetu, vilevile tunapenda kumshukuru Mhe. Mbunge Angelina S. Mabula kwa kuendelea kuchochea na kuhamasisha utekelezaji wa Miradi katika Halmashauri yetu, pia tunamshukuru Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, Waheshimiwa Madiwani, Wenyeviti wa Mitaa, Watumishi wote wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela na Wananchi wote kwa ujumla kwa kuendelea kutoa ushirikiano kwa ajili ya kuendelea kutekeleza Miradi ya Manispaa ya Ilemela.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Naomba kuwasilisha.

Ummy M. Wayayu

**MKURUGENZI WA MANISPAA YA ILEMELA**



CamScanner

iii. Shilingi 262,369,781.70 kwa ajili ya Mfuko wa Wanawake, Vijana na watu wenye Ulemavu

iv. Shilingi 180,000,000.00 kwa ajili ya ukamilishaji wa Wodi ya Wazazi Zahanati ya Nyakato

v. Shilingi 136,167,966.85 kwa ajili ya fidia ya Ardhi

vi. Shilingi 118,000,000.00 kwa ajili ya malipo ya greda awamu ya kwanza

vii. Shilingi 100,000,000.00 kwa ajili ya malipo ya Mkandarasi wa ujenzi wa barabara ya Hospitali ya Wilaya

viii. Shilingi 70,000,000.00 kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa kituo cha Afya Kayenze

ix. Shilingi 70,000,000.00 kwa ajili ya ununuzi wa eneo kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Nyasaka

x. Shilingi 40,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa uzio Shule ya Misingi Kitangiri

xi. Shilingi 37,500,000.00 kwa ajili ya malipo ya kijiko(mtambo) awamu ya kwanza

xii. Shilingi 72,505,000.00 kwa ajili ya ukamilishaji wa Hosteli ya wanafunzi wenye mahitaji maalum S/M Buswelu

xiii. Shilingi 30,000,000.00 kwa ajili ya uendelezaji wa ujenzi wa Ofisi ya Kata ya Nyasaka

xiv. Shilingi 30,000,000.00 kwa ajili ya Umaliziaji wa Maabara Zahanati ya Kahama

xv. Shilingi 25,000,000.00 kwa ajili ya umaliziaji wa madarasa 2 Kiloleli S/M

xvi. Shilingi 37,500,000.00 kwa ajili ya umaliziaji wa madarasa 3 Umoja S/M

xvii. Shilingi 25,000,000.00 kwa ajili ya ukamilishaji wa madarasa 2 Bugogwa S/M

xviii. Shilingi 25,000,000.00 kwa ajili ya umaliziaji wa madarasa 2 Lumala Sekondari

xix. Shilingi 25,000,000.00 kwa ajili ya uendelezaji wa Zahanati Bwiru

xx. Shilingi 24,000,000.00 kwa ajili ya umaliziaji wa madarasa 3 Shule ya Sekondari Mnarani

xxi. Shilingi 22,800,000.00 kwa ajili ya uendelezaji wa ujenzi Ofisi ya Kata ya Mecco

xxii. Shilingi 21,000,000.00 kwa ajili ya matengenezo ya mitaro Eneo la makaburi Kata ya Buzuruga.

xxiii. Shilingi 20,000,000.00 kwa ajili ya umaliziaji wa choo, incinirator na Placenta pit katika Zahanati ya Kawekamo

xxiv. Shilingi 20,000,000.00 kwa ajili ya umaliziaji wa Ofisi ya Mtaa wa Kilimahewa "A

xxv. Shilingi 20,000,000.00 kwa ajili ya uendelezaji wa nyumba ya Mwalimu Bezi S/M



CS CamScanner

xxvi. Shilingi 20,000,000.00 kwa ajili ya uendelezaji wa Jengo la mama na mtoto Zahanati ya Luhanga

xxvii. Shilingi 20,000,000.00 kwa ajili ya kuanza kazi za umaliziaji wa zahanati Nyambiti

xxviii. Shilingi 20,000,000.00 kwa ajili ya uendelezaji wa Zahanati ya Lubala

xxix. Shilingi 19,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa choo shule ya Msingi Mkudi

xxx. Shilingi 19,000,000.00 kwa ajili ya utengenezaji wa barabara ya mawe Kigoto

xxxi. Shilingi 15,000,000.00 kwa ajili ya umaliziaji wa Ofisi ya Mtaa Kabusungu

xxxii. Shilingi 15,000,000.00 kwa ajili ya umaliziaji wa Ofisi ya Mtaa Nenetwa

xxxiii. Shilingi 12,000,000.00 kwa ajili ya umaliziaji wa madarasa 3 Shule ya Msingi Bujingwa

xxxiv. Shilingi 11,000,000.00 kwa ajili ya umaliziaji wa Ofisi ya Mtaa wa Nyashimba

xxxv. Shilingi 10,000,000.00 kwa ajili ya Umaliziaji wa nyumba ya Mwalimu Nyamhongolo S/M

xxxvi. Shilingi 9,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa choo katika soko la Omary

xxxvii. Shilingi 6,200,000.00 kwa ajili ya umaliziaji wa jengo la mama na mtoto Zahanati ya Chamwenda

xxxviii. Shilingi 25,000,000.00 kwa ajili ya ukamilishaji wa chumba cha X-ray kituo cha Afya Buzuruga

xxxix. Shilingi 24,000,000.00 kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa shule ya Sekondari Angelina Mabula

xl. Shilingi 10,445,832.00 kwa ajili ya ununuzi wa madawati 150 kwa ajili ya Shule za Misingi na kugawanywa shule za Msingi Nsumba (50), Buswelu (50) na Buyombe (50).

xli. Shilingi 7,964,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa choo kipya na ukarabati wa choo cha zamani katika uwanja wa Furahisha

xlii. Shilingi 3,900,000.00 kwa ajili ya ununuzi na upandaji Miti 1500

xliii. Shilingi 25,000,000.00 kwa ajili ya ukamilishaji wa vyumba 2 vya madarasa Shule ya Msingi Magaka.

xliv. Shilingi 25,000,000.00 kwa ajili ya ukamilishaji wa madarasa 2 Shule ya Msingi Chasubi

xlv. Shilingi 23,954,000.00kwa ajili ya ununuzi wa viti na meza 350 kwa shule za Sekondari na kupelekwa shule za Sekondari Kabusungu (200), Kisenga (50), Lubuka (100)



CamScanner

xlvi. Shilingi 23,010,000.00 kwa ajili ya ununuzi wa madawati 325 katika shule za msingi awamu ya kwanza na kupelekwa Shuleza Msingi Nsumba (50), Buyombe (50), Buswelu (50), Karume (25), Kirumba(25), Mnarani (25), Kahama (50), na Nyamadoke (50)

xlvii. Shilingi 18,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa vyoo shule ya Sekondari Bujingwa

xlviii. Shilingi 18,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa vyoo shule ya Sekondari Ibinza

xlix. Shilingi 14,000,000.00 kwa ajili ya ukamilishaji wa vyoo shule ya Msingi Ibungilo

l. Shilingi 14,000,000.00, kwa ajili ya ukamilishaji wa vyoo shule ya Msingi Isesa

**KIAMBATANISHO B**

**SERIKALI KUU**

vii. Shilingi 584,280,209.00 kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya ya Sekondari Masemele

viii. Shilingi 584,280,209.00 kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya ya Sekondari Kilabela

ix. Shilingi 351,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa Shule ya Msingi mpya ya mkondo mmoja Masemele



CamScanner

x. Shilingi 260,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa Mabweni 2 katika shule ya Wavulana Bwiru
xi. Shilingi 155,500,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 2 ya awali ya mfano, matundu 12 ya vyoo, vyumba 3 vya madarasa Shule ya Msingi Kayenze Ndogo
xii. Shilingi 100,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa Nyumba ya mwalimu (2 in 1) katika shule ya Sekondari Kisenga
xiii. Shilingi 92,410,714.29 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya mtumishi wa Afya Zahanati ya Bezi mtaa wa Tefu
xiv. Shilingi 92,410,714.29 kwa ajili ya ujenzi wa OPD mtaa wa Bezi
xv. Shilingi 92,410,714.29 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya mwalimu ya familia mbili mtaa wa Iseni Kayenze sekondari
xvi. Shilingi 92,410,714.29 kwa ajili ya ujenzi wa OPD Zahanati ya Luhanga Kata ya Kiseke
xvii. Shilingi 87,158,076.29 kwa ajili ya ujenzi wa bweni la wavulana 80 shule ya sekondari Kayenze kuanzia msingi hadi upauaji mtaa wa Kayenze
xviii. Shilingi 77,278,611.61 kwa ajili ya ujenzi wa bweni la wavulana 80 shule ya sekondari Kayenze kwa hatua ya umaliziaji mtaa wa Madukani
xix. Shilingi 300,000,000.00 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba katika Hospitali ya Wilaya
xx. Shilingi 239,000,000.00 kwa ajili ya ukamilishaji wa Hospitali ya Wilaya
xxi. Shilingi130,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa bweni shule ya Sekondari Bwiru Wavulana
xxii. Shilingi 113,396,000.00 kwa ajili ya ukamilishaji wa Bwalo Shule ya Sekondari Sangabuye
xxiii. Shilingi 100,000,000.00 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba Zahanati
xxiv. Shilingi 83,761,000.00 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi kupitia fedha za Mfuko wa Jimbo.



CamScanner